# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL8

# KISWAHILI PAPER 3 ANSWER

## SEHEMU YA A (Alama 20 )

### TAMTHILIA

1. (a) Msemaji ni Meya.Anamsea Bili.Ni ofisini mwa Meya.Bili anazua mpango wa kusitisha kandarasi ili Meya alazimishwe kumlipa mwanakandarasi fidia.Meya atapata mgao wake kwa fidia hivyo.Meya akipata naye asimsahau Bili (4x1=4)
(b) Mbinu za kifasihi katika dondoo. (i) Balagha- Nilikusahahu lini? (ii) Msemo/Nahau-kukata mkono *Mbinu 1 mk mfano 1 mk (1x2=2)
(c) Hulka ya Bili.
(i) Mwenye tamaa-alimshauri Meya kuhusu kandarasi ambayo ingewaletea pesa//alimshauri Meya kuuza fimbo ili wapate pesa
(ii) Mwenye ubinafsi –alijitakia faida yake mwenyewe n.k. (zozote 2x2=4)

(d) Jinsi Wanacheneo walivyokata mkono anaowalisha.

(i) Meya kuchelewesha mishahara ya wafanyakazi.

(ii) Meya kulipa wafanyakazi mishahara duni.

(iii)Meya kukosa kupatia Wanacheneo huduma za afya licha ya kuwa wao ndio Waliomchagua.

(iv) Uongozi kutowapa Wanacheneo vyakula ilhali Meya mwenyewe anakula vinono.

(v) Wafanyakazi kutozwa kodi ilhali Meya na madiwani hawalipi kodi.

(vi) Vijana kutopewa kazi.walipewa ahadi za uongo ilhali ndio waliochagua viongozi.

(vii) Wafanyakazi kufanya kazi katika mazingira magumu, mfano kukosa glavu.

(viii) Wafanyakazi wanaogoma kwa kudai mazingira bora ya kazi kufurushwa kazi na kuuawa kwa kupigwa risasi.

(ix) Waridi kutohudumia wagonjwa ilhali wao hulipa kodi ili naye alipwe mshahara.

(x) Bili kumtoroka Meya mambo yalipoharibika.

(xi) Mhazili wa Meya kumtoroka na kuungama na wanaogoma licha ya Meya kumpa ajira.

(Zozote 9x2=18)

## SEHEMU YA B: (Alama 20 )

### RIWAYA

2. 2. (a)

- Aliwatazama Bi.Zuhura na Amani.

- Ni nyumbani mwa Mtemi Nasaba Bora katika chumba cha malazi.

- Mtemi Nasaba Bora aliwafumania wawili hao katika chumba cha malazi.

Bi Zuhura alikuwa amemwita Amani.Mtemi alifikia uamuzi kuwa

Bi.Zuhura na Amani walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Alimpiga Amani vibaya sana. (4x1=4)

(b) Hulka ya mrejelewa (Nasaba Bora)

(i) Laghai –alificha faili za watu ili apate hongo.

(ii) Fisadi-alighushi hatimiliki za mashamba.

(iii) Katili –alimuua Chirchir Hamadi na kupokonya jamii yake shamba.Alimpiga Amani kikatili na kumtupa.

(iv) Mwenye tamaa-alipokonya watu mashamba k.m Chirchir Hamadi na familia ya Imani.

(v) Mwenye mapuuza –Hakutunza nyumba wala mazingira yake.

(vi) Mwongo –eti alienda kusuluhisha migogo ya mashamba.

(vii) Msinzi-Alihusiana na Lowela. *Mtahini ahakiki hoja zingine) (zozote 3x2=6)

(c) Mchango wa wanawake.

- Walezi – Imani alilea watoto wa Majisifu.

Bi Dora alilea watoto wake.

Bi. Zuhura alisaidia kulea kitoto Uhuru.

- Wasaidizi- Imani alisaidia Amani safari ya kuenda Sokomoko.

- Wasahemevu- Imani alimsamehe Nasaba Bora licha ya maovu aliyomtendea.

-Wazinifu/washerati- Lowela na Mashaka walijihusisha na wanaume wakiwa shuleni.

- Wakarimu- Bi. Zuhura alimkaribisha Amani, Imani na kitoto Uhuru kwake.

- Viongozi- Imani alimsaidia Amani katika uamuzi wa kutohudhuria sikuku ya wazalendo.
-Wavumilivu- Bi. Dora na Bi. Zuhura walivumilia mateso katika ndoa zao.

- Wavivu- Bi. Zuhura anaishi katika nyumba chafu na viti pia ni vichafu.

-Watetetzi- Imani alitetea mama yake dhidi ya kupigwa na askari.

- Wenye Imani- Imani alikunywa maji ya Mto Kiberenge na kubadilisha Imani ya wengi kuhusu maji yam to huo. (Zozote 5x2=10) * Mtahini ahakiki majibu mengine.

3. **A Matumizi ya majazi.**
1. Nasaba Bora –Mtemi alitoka katika ukoo wenye hadhi.Babake alikuwa kasisi Mudir wa Wilaya alikuwa mtu wa akraba yake.Alijiona bora kuliko Majisifu.Yeye ni miongoni mwa Waafrika wachache waliorithi vyeo na mali ya wazungu.
2. Majisifu –majigambo/maringo.Alijiona mwandishi mtajika.Alijiona bora katika sarufi.Alimringia Dora kuwa angenyakuwa tuzo ya Fasihi.
3. Madhubuti-Ni kitu kuwa imara, hakitetereki.Madhubuti alikuwa na msimamo imara.Alikataa kazi aliyetafutiwa na babake.Alikana Nasaba yake.Alihamia kwa Amani.

4. Mashaka-Ni taabu au mateso.Uchumba wake na Ben Bella unavunjika, anakuwa wazimu.Alihusiana na Ben Bell ambaye alikuwa mfungwa sugu wa jela.

5. Amani-Ni hali ya utulivu au usalama.Alitafuta kusuluhisha matatizo yake kwa Amani.Alikaa na watu kwa Amani k.m Nasaba Bora na Imani.Alimsamehe Majisifu.Alimkinga Nasaba Bora dhidi ya

kuuawa na Oscar Kambona.

6. Imani –kuamini kuwa jambo ni la kweli au kwamba litatendeka.Pia inamaanisha kuwa na huruma.Aliandamana na Amani kwenda Sokomoko kwa kuamini kuwa Amani ni mtu mwema.Alikunywa maji ya mto Kiberenge na kuamini kuwa hayangemdhuru.Aliamini kuwa Amani hakuwa na uhusiano wa kimapenzi na Bi.Zuhura.Aliwahurumia watoto walemavu wa Majisifu.

7. Matuko Weye- kituko ni jambo lisilo la kawaida.Mhusika huyu ni mwendawazimu.Alivuruga mkutano wa Nasaba Bora.Alivaa kaptura juu ya suruali.Alikula kitoweo kwanza. Alikula chakula alichopewa bila kutoa shukrani.

8. Uhuru –Ni hali ya mtu kupewa mamlaka ya kujitawala.Kitoto Uhuru kilizaliwa wakati Wanasokomoko wanaadhimisha siku ya kupata uhuru.

(zozote 5+ maelezo 2=10)

*Mtahini ahakiki majibu mengine.

**B. Matumizi ya kinaya.**

1. Nasaba Bora anawafuta kazi wafanyakazi wanaponadhifisha kasri badala ya kuwadumisha kazini.

2. Uso wa Imani unasemekana kuwa na tabasamu siku zote.Hata hivyo moyoni alikuwa na fundo chungu.Imani kuwa kwao kungeenda vyema haikufanyika.

3. Ni kinaya Majisifu kushiriki ulevi na kupuuza dini ilhali babake alikuwa kasisi.

4. Ni kinaya Amani kumwokoa Nasaba Bora na mashambulizi ya Oscar Kambona ilhali alikuwa adui yake mkubwa.

5. Jina la Mtemi Nasaba Bora ni kinyume na hulka yake.Yeye alitenda mambo mabaya kwa mfano alikuwa na jicho nje, kudhulumu n.k.

6. Ni kinaya kwa Mashaka kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Ben Bella huku akielewa kuwa Ben Bella ni jangili.

7. Ni kinaya Mitchelle kutaka ajengewe nyumba na Major Noon lakini baada ya kujengewa ilikataa eti idadi ya vyumba ilikuwa witiri.

8. Ni kinaya Madhubuti kukataa kazi aliyotafutiwa na babake.Alikataa kujitambulisha na jina la babake.

9. DJ anahurumia lile jibwa kwa kufungwa na linakuja kumuuma baadaye

10. Majisifu ana elimu nzuri lakini anaishi kuwa mraibu sugu wa pombe haramu ilhali ameacha pombe ya chupa nyumbani.
11. Nasaba Bora anamtaliki mkewe kwa tuhuma kuwa yeye ni mzinifu ilhali yeye alikuwa mpenzi wa Lowela. 12. Nasaba Bora alizaa mtoto na Lowela na kumsukumia Amani ili amlee. (zozote 5x2=10)

# SEHEMU YA C (Alama 20 )

## HADITHI FUPI

# SEHEMU YA D (Alama 20 )

## USHAIRI

4. (a) Ufaafu wa anwani "Ndoa ya samani".

Abu alipotaka kuoa Amali, wazazi wa Amali walitaka Abu awanunulie samani kabla yao kuoana.Hivyo basi anwani ni faafu. (alama 2)

(b) Maudhui katika "Ndoa ya samani"

1. Matabaka. - Watu huoana kulingana na daraja ya matabaka yao.Abu anakataliwa kumwoa Amani kwa kuwa Abu anatoka daraja la kati.

2. Umaskini. - Hapo mwanzo Abu na familia yake walikuwa maskini wa kupigiwa mfano.Walikosa mahitaji ya kimsingi.Tajiri atapendwa

3. Ubinafsi. Wazazi wa Amali walitaka mipango yote ya arusi ifanyiwe kwao na siyo nyumbani mwa Abu.

4. Juhudi katika kazi. Abu alifanya kazi kwa bidii.Alianza kufanya vibarua.Hakuchagua kazi. Mwishowe alifanya kazi Uarabuni na kupata utajiri.

5. Nafasi ya wazazi. - Wazazi wa Amali waliamua kuwa Amali hataolewa kwa Abu.Waliona kuwa hangeweza mahari.Abu alipokuwa tajiri, pia wakaamua kuwa Amali aolewe na Abu.

6. Mila na destri.

- Abu alienda na mjombake kupeleka posa.

- Desturi ya mahari ilimkosesha Abu ndoa.

- Bwana arusi alitozwa kiingilio kabla ya kumfikia Bi.Arusi.

- Nyimbo za arusi zenye maana fiche ziliimbwa.

7. Tabia njema.

- Abu alikuwa na tabia njema.Alipokuwa tajiri hakuwa na kiburi kama matajiri wengine.Aliwakumbuka marafiki wenzake.Aliwajengea ndugu zake na wazazi wake nyumba.

8. Akiba.

- Abu alifanikiwa kuwa tajiri mkubwa kutokana na kuweka akiba.

9. Nafsi ya mwanamke.

- Mwanamke (Zena –mamake Amali) amechorwa kama kikwazo cha mafanikio.Alikataa Amali asiolewe na Abu kwa sababu ya umskini. (Hoja 9x2=18) *Mtahini ahakiki hoja zingine.

5. (a) Maneno haya yalisemwa na Bi.Margaret /mkuu wa shule ya upili ya Mtakatifu

Timotheo.√Alikuwa ofisini mwake. √Alikuwa anawaambia wazazi wa Sela. (Bw na Bi Butali)

√Walifika kujua sababu ya binti yao kufika nyumbani kuwachukuwa, √ (4x1=4)

(b) –Sista (mwuguzi wa shule) alifanyia wanafunzi uchunguzi. Matokeo yalionyesha kuwa Sela alikuwa na mimba.Sela alishika urafiki na Chris Masazu wakati wa siku ya michezo shuleni mwa Sela.Sela alifukuzwa nyumbani ili kuwaita wazazi wake. (alama 4)

(c) Changamoto za jinsia ya kike:

1. Kudhulumiwa kimapenzi k.m Sela.

2. Kutwikwa mzigo wa malezi ya wanao k.m Mama Sela.

3. Kuathirika kimasomo k.m Sela alifunzwa shuleni.

4. Kutalakiwa bila sababu mahsusi k.m Mama Sela. (hoja 4 zenye ufafanuzi 3=12)

6. (a) Kibali/ruhusa/idhini/uhuru.

(i) Inkisari-walo badala ya walio,n.k.

(ii) Kikale/kizamani/lahaja-mbwako=wako.

(iii)Tabdila-watakushutuma=watakushitumu,duniya=dunia n.k Kuboronga sarufi-sema kwa yako mighani=sema kwa maghani yako n.k

(iv) Utohozi=Noleji=knowledge.

(v) Mazda/mazida-radidia n.k (zozote 2x1=2)

(b) Bahari.

(i) Tarbia/unne –mishoro minne kila ubeti.

(ii) Mathnawi-vipande viwili(ukwapi na utao)
(iii)Sabilia-kibwagizo kina badilikabadilika.

(iv) Kikwamba-neno "sema"linaanza mishororo yote.

(v) Pindu/nyoka/kikufu-neno sema linakamilisha mshororo wa tatu na kuanza mshororo wa nne.

(vi) Ukara-vina vya utao vinatiririka/vinafanana/vinaendelezwa lakini vina vya ukwapi havititririki/havifanani/haviendelezwi.

(vii) Kikai-idadi ya mizani hailingani,ukwapi ni mingi (8) kuliko ya utao (6) (zozote 4x1=Hoja + mfano =4)

(c) Usambamba wa kiusawe. Ni matumizi ya maneno tofauti kuelezea jambo lile lile (maneno yenye maana sawa) k.m Sema-longa, noleji-hekima, n.k. (alama 2)

(d) Toni –ina uchungu/hasira/ukali (alama 2)

(e) Nafsi neni-

(i) Mdhulumiwa.

(ii) Anayedhulumu. (2x1=2)

(f) Sifa za kiarudhi.

(i) Mishororo –minne/tarbia/unne.

(ii) Vipande –viwili/ukwapi na utao.

(iii)Vina –shairi lina vina.

(iv) Mizani –mizani inalingana kila ubeti 8,6 8, 6 8, 6 8, 6

(v) Kibwagizo –shairi lina kibwagizo. (zozote 4x1=4)

(g) Lugha nathari /tutumbi/sufufu.

-Taja hila na udanganyifu wote unaowapambaza watu duniani.

-Taja maovu yote ambayo yamewanasa watu.

-Dunia ni mahali hatari kwani anayejiingiza kwenye malimwengu hujuta.

-Yaseme maovu yote. (alama 4)

*Mtahiniwa ajiepushe na mishororo, inkisari,tabdila,kuboronga sarufi. n.k

## SEHEMU YA E (Alama 20 )

### FASIHI SIMULIZI

5. (a) Videndawili: ni semi muundo wa swali ambazo huhitaji jibu. (alama 2)

(b) Aina ya vitendawili:

(i) Vitendawili sahili: Huwa na sentensi moja.

(ii) Vitendawili tata: Huhitaji akili kujibu.

(iii)Vitendawili visimulizi: Husimulia hadithi.

(iv) Vitendawili tanakali: Hutumia tanakali za sauti.

(v) Vitendawili mkufu:vina sehemu mbili zinazohusiana

k.m Nikitembea yupo.Nikiingia kwa nyumba hayupo:Jibu –kivuli. (zozote 3+ maelezox2=6)

(c) Sifa za vitendawili

(i) Huwa mwanzo maalum k.m "Kitendawili"

(ii) Huwa na wahusika zaidi ya mmoja.

(iii)Vina ujumbe wa kimafumbo.

(iv) Huwa na ufupi wa kimaelezo.

(v) Kuna vitendawili vya neno moja.

(vi) Kuna vitendawili vya takriri/urudiaji.

(vii) Vitendawili hubadilika na wakati na mazingira.

(viii) Hutegwa na kuteguliwa jioni.

(ix) Kuna vitendawili vya sauti pekee.

(x) Kuna vitendawili vya maumbo mafupi na marefu. (zozote 5x1=5)

(d) Majukumu ya vitendawili.

(i) Hupanua ujuzi wa watoto.

(ii) Huelimisha/hufundisha.

(iii)Hukuza uwezo wa kufikiri/chemsha bongo.

(iv) Hukuza lugha.

(v) Huhifadhi historia na utamaduni wa jamii.

(vi) Huburudisha/huchangamsha/hufurahisha.

(vii) Ni kichocheo cha udadisi na utafiti.

(viii) Hupitisha ujumbe maalum.

(ix) Hutazamisha mazingira.

(x) Hukuza lugha.

(xi) Hukuza ushirikiano.

(xii) Kukuza uwezo wa kukumbukia. (zozote 7x1=7)